

Kazi ya shirika la Survivor Alliance

Kuunganisha na kuwatia nguvu kote ulimwenguni, waathirika wa utumwa na wa usafirishaji haramu wa binadamu.

Misimamo ya Uanachama wa shirika wa Survivor Alliance

Tafadhali soma kila moja ya taarifa hizi kwa uangalifu. Tunaomba kwamba washiriki wote ambao wanataka kujiunga nasi kuzingatia haya kama misimamo yetu ya msingi.

Musimamo wetu ni mtu kuzungumza na mwengine wala sio mtu kuzungumuza pahali pa mwengine.

Sisi sio "sauti za wasio na sauti". Kila mmoja wetu ana sauti. Wamoja hujielezea kwa njia ya kuzungumza mbele ya watu, wengine kwa njia ya kuandika, wengine tena kupitia utendaji wa pamoja na jamii, na wengine kupitia vituo vya ubunifu kama sanaa au picha. Tunazungumza kutokana na tulio wahi kuyapitia maishani na tunatiana nguvu sisi kwa sisi ili kuwezesha kusikilizwa.

Tunakubaliana kuwa tulio wahi kuyapitia maishani ni ya pekee na inatofautiana.

Tunakubaliana na ukweli kwamba ufafanuzi unao tolewa na Shirika la Umoja wa Mataifa kuhusu usafirishaji haramu wa binadamu ni pana na kwamba aliyo wahi kuyapitia kila aliyenusurika hayawezi kuwakilisha aina zote na mienendo ya usafirishaji haramu wa binadamu. Kwa hivyo, tunajitahidi kuungana ili kuelimishana kuhusu utofauti ulioko katika ya yale tulio wahi kuyapitia na pia kuunganisha kila aliyenusurika na kila fursa inayo ambatana hasa na hali yake kwa upekee.

Tunaamini kuwa matumizi ya neno "sisi" ina nguvu kuliko matumizi ya neno "mimi".

Tokana na kwamba kundi la Walio Nusurika ni kubwa kiasi hiki na linamo watu wenye kuwa na tofauti zao kiasi hiki, huenda isiwe kwamba ni kila wakati ndio tunapokubaliana kuhusu maoni. Walakini, tunapokubaliana, sauti ya pamoja itaturuhusu kuweka shinikizo kwa nanao chukuwa maamuzi ya sheria, ili kusimama pamoja dhidi ya udhalimu, na kuweza kukusanya rasilimali pamoja, na mambo mengine kama na hayo.

Tutayapa kipaumbele yanayohusu afya na ustawi wetu kwanza.

Tunatambua umuhimu wa kuongoza kwa kuwa kielelezo kwa wengine. Ili kuwa viongozi bora, wanaharakati, washauri, na wanajamii, tutatoa kipaumbele kwanza kwa afya na ustawi wetu.

Tutakuza kutumia utaratibu unao weka maanani hali inayo weza kuletwa na majeraha ya ndani ya mioyo.

Tunatambua kuwa matukio ya majeraha ya ndani ya mioyo (kiwewe) hutokea hapa na pale ulimwenguni kote. Kwa hivyo, tunatambua kwamba mtu yeyote, sio tu manusura wa biashara ya binadamu, anaweza athirika na hali inayo baki kwa muda murefu huku ikiwa imetokana na majeraha yalio tokea ndani ya moyo. Kwa hivyo, tutakuza kutumia taratibu inayo weka maanani hali ya vidonda vya ndani ya moyo kila kunako husika vikao, na hii ikiwemo na hasa katika mkutano wowote unaohusisha waathirika wa biashara ya binadamu.

Tutakuza umoja na kujilinda dhidi ya mgawanyiko.

Tokana na kwamba kundi la Walio Nusurika ni kubwa kiasi hiki na linamo watu wenye kuwa na tofauti zao kiasi hiki, tunaielewa kuwa hali ya kuwa ya watu na matazamio kati yao yaweza kutokukubaliana. Zaidi ya yote, tutapata msingi wa pamoja kuhusiana na unyanyasaji tulio wahi kuupitia na kuhusiana na lengo letu la kuzuia bihashara haramu ya binadamu, na pia kuhusiana na kuwalinda wahanga, na kuwapa nguvu waathirika. Tunatarajia kila mtu kukuza umoja na kujilinda dhidi ya mgawanyiko.

Tunajitolea kufanya kazi katika kupitia changamoto na mizozo kwa njia ya heshima.

Tunaamini kuwa tofauti katika mitazamo ni jambo la linalo tokea na lenye kufaidia. Walakini, wakati changamoto na mizozo zinapoibuka, tutajibu kitaalam na kutafuta kuyatatua kwa njia ya kinidhamu na ya heshima. Hatukuzi utamaduni wa "kuita walio nje". Tunahimiza waathirika kuzungumuza moja kwa moja kuhusu kutokukubaliana. Ikiwa mzozo hauwezi kutatuliwa, tunatarajia wahusika wote waendeleo kuishi kwa ustadi na kwa urafiki.

Tunatambua kuwa kila mtu ana jukumu muhimu katika harakati za kupambana na hali ya kuwafanya binadamu kuwa biashara.

Tunaamini kwamba manusura wote wanaweza kuchukua jukumu katika harakati za kupambana na hali zinazo wafanya binadamu kuwa biashara.

- hakuna sharti kwa yeyote kujiweka hazarani. Kila aliyenusurika yuko binafsi kwenye safari ya kipekee na lazima aamue mwenyewe jinsi, au ikiwa, anataka kujihusisha.